MAZUNGUMZO YA UMOJA

Ukosoaji na Usahihishaji

Kimeandikwa na:
Sheikh Hassan Musa al-Saffar

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 1 10/26/2015 1:14:47 PM

ترجمة

خطاب الوحدة
نقد و تقويم

تأ ليف
الشيخ حسن بن موسى الصفار

من اللغة العربية الى اللغة السواحلية

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 2 10/26/2015 1:14:48 PM

©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:
AL-ITRAH FOUNDATION

ISBN: 978 - 9987 – 17 – 029 – 6

Kimeandikwa na:
Sheikh Hassan Musa al-Saffar

Kimetarjumiwa na:
Abdul- Karim Juma Nkusui
abdulkarimjuma@yahoo.com

Kimehaririwa na:
Alhaji Hemedi Lubumba

Kimepitiwa na:
Mbarak A. Tila

Kimepangwa katika Kompyuta na:
Al-Itrah Foundation

Toleo la kwanza: Machi, 2016
Nakala: 2000

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Alitrah Foundation
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640 / 2127555
Barua Pepe: alitrah@yahoo.com
Tovuti: www.ibn-tv-com
Katika mtandao: w.w.w.alitrah.info

YALIYOMO

Neno la Mchapishaji 1

Utangulizi..... 6

Mazungumzo ya Umoja Ukosoaji na Usahihishaji..... 5

Katika Upande wa Asasi za Kiraia..... 11

Uwezo wa Kuathiri 14

Kukubali Wingi wa Madhehebu 17

Kujengea Dhana Mpya 27

Kupanga Msimamo..... 30

Ufuatiliaji wa Matangazo..... 32

Maulamaa: Mazungumzo ya Kiislamu
Yanakabiliwa na Tatizo 32

Mwanachuoni wa Kidini wa Kishia wa Saudia
Ashutumu Siasa za Ubaguzi 38

Rejea 41

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 4 10/26/2015 1:14:48 PM

بسم الله الرحمن الرحيم

Kwa jina la Mwenyezi Mungu,
Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.

Sifa zote njema anastahiki Mola Mlezi wa viumbe. Ewe Mwenyezi Mungu msalie Muhammad na kizazi cha Muhammad kama ulivyo msalia Ibrahim na kizazi cha Ibrahim, na mbariki Muhammad na kizazi cha Muhammad kama ulivyombariki Ibrahim na kizazi cha Ibrahim, hakika wewe ni mtukufu mwenye kuhimidiwa.

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 5 10/26/2015 1:14:48 PM

DIBAJI

Kitabu hiki ni toleo la Kiswahili la taasisi ya Al Itrah Foundation. Chapisho lake limelenga kukidhi mahitaji ya kiroho ya zama hizi pamoja na Ubongo na fikra zinazokuwa za Muislam. Jitihada kubwa zimefanywa na Taasisi kuweka chapisho hili la Kiswahili katika msingi wa haki na wenye kukubalika katika Uislam.

Unaombwa kwa Taadhima ukisome kitabu hiki katika malengo yaliyokusudiwa. Pia Unaombwa kuwasilisha kwetu maoni yako huru juu ya chapisho letu hili, jambo ambalo tutashukuru sana.

Kutangaza ujumbe wa Uislam ni kazi ambayo inahitaji ushirikiano wetu sote. Taasisi inakuomba kuungana na kushirikiana kama ilivyoagizwa katika aya ya Qur'an: (Surat Saba' 34:46).

Na rehma za Allah ziwe juu yako.

Wako katika Uislam

Al Itrah Foundation

Barua Pepe: alitrah@yahoo.com

SMS: +255 778 300 140

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 6 10/26/2015 1:14:48 PM

بسم الله الرحمن الرحيم

NENO LA MCHAPISHAJI

Mazungumzo ya Umoja - Ukosoaji na Usahihishaji ni kitabu kinachotoa mwongozo wa jinsi ya kujadiliana katika hali nzuri ya kuamiliana na kuheshimiana baina ya madhehebu na baina ya dini mbalimbali.

Kitabu hiki asili yake ni khutba aliyoitoa Sheikh Hasan Musa as-Saffar katika kongomano lililofanyika katika kitivo cha masomo ya Kiislamu katika Chuo Kikuu cha Qatar, na kitivo cha sharia na masomo ya Kiislamu katika Taasisi ya Qatar ya malezi na sayansi. (Maelezo zaidi soma utangulizi wake)

Madhumuni ya mijadala ya Sheikh as-Saffar ni kujaribu kuondoa wingu kubwa lililoigubika mijadala yetu ambayo imekuwa ya kukashifiana, kutukanana, kukufurishana n.k., badala ya kuelimishana, kufahamiana, kuamilana na kujenga umoja wa Waislamu.

Sheikh wetu huyu amechukuwa fursa hii ili kujaribu kuleta muamala mzuri baina ya madhehebu hususan za Kiislamu na dini nyingine kwa ujumla.

Umoja wa Waislamu ni muhimu sana, na wakati huu suala hili linazidi kuwa na umuhimu mno. Tangu zamani kumekuwepo kutokuelewana kusiko kuwa na maana kati ya madhehebu mbili kubwa za Kiislamu - Sunni na Shia. Katika baadhi ya sehemu hali hii mbaya ilishadidi kiasi cha kufikia wafuasi wa kila madhehebu kuona kwamba ni halali kumwaga damu ya mfuasi wa madhehebu nyingine.

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 1 10/26/2015 1:14:48 PM

Hali hii haipwasi kuachwa iendelee, lazima wajitokeze viongozi wa kila madhehebu kulikemea na kulitafutia ufumbuzi. Kwa hakika wako viongozi katika kila upande ambao huutakia mema Uislamu wetu, ambao hawataki malumbano juu ya hitilafu zilizopo kati ya madhehebu zao. Kwao hitilafu hizo ni ndogo sana na kwamba mambo ambayo yanawaunganisha ni mengi zaidi ambayo ndiyo mambo ya msingi katika Uislamu, kinyume na yale machache wanayohitalifiana ambayo sio ya msingi katika Uislamu. Mathalan, wote wanakubaliana katika misingi mikuu mitatu ya Uislamu – Tawhidi, Utume na Kiyama. Wote wanasali sala tano za kila siku, wote wanafunga mwezi mtukufu wa Ramadhani, wote wanatoa zaka, wote wanakwenda kuhiji, wote wanaposali huelekea Kaaba, wote wanasoma Qur'ani moja, wote Mtume wao ni mmoja Muhammad (s.a.w.), na kwamba wote wanaamini kwamba Muhammad ni Mtume wa mwisho hatakuja Mtume mwingine baada yake, wa mwanzo wao akiwa ni Nabii Adam (a.s.). Haya ni machache katika mengi wanayokubaliana. Hivyo viongozi wa kidini kwa busara zao huaangalia yale tu mengi yanayowaunganisha na kujishughulisha nayo na kuachana na yale machache ambayo huhitalifiana ili kuleta mkuruba na umoja katika Uislamu.

Hapa lazima ieleweke kwamba umoja tunaouzungumzia sio wa kuziyeyusha madhehebu, la si hivyo, bali tunazungumzia umoja wa Waislamu wenyewe katika masuala yanayohusu Uislamu, kama alivyoandika haya Marehemu Sayyid Saeed Akhtar Rizvi katika kitabu chake kiitwacho, Maswali Yako Yajibiwa, (Kitabu cha Tano) katika kujibu swali la nam. 61:

Swali: Je, tunapaswa kutangaza imani zetu za madhehebu wakati Iran ina kampeni ya umoja wa Kiislamu? Je, ni lazima tuendeleze (kulingania) madhehebu yetu kwa Masunni au inatubidi kujiepusha

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 2 10/26/2015 1:14:48 PM

kwa ajili ya umoja? Kama ni hivyo, umoja lazima uwe wa ndani na wa karibu, au wa juu juu tu?

Jibu: Inaonekana kujitokeza kutokueleweka kuhusu kaulimbiu ya Iran ya "Umoja wa Kiislamu" kwa wote Shia na Sunni. Kuna uwezekano wa njia tatu wa umoja miongoni mwa Waislamu. Mbili kati ya hizo ni:

1. Muungano katika imani - kwamba Waislamu wote wafuate imani za madhehebu moja, au

2. Umoja katika hukumu za Sharia - kwamba Waislamu wote wafuate taratibu za kiibada za madhehebu moja, ziwe ya kibinafsi, kijamii, kifedha au sheria za adhabu.

Kwa dhahiri njia zote hizi mbili haziwezekani kufuatwa. Sasa imebakia tu njia ya tatu ya muungano, nayo ni muungano katika kukabiliana na maadui wa Uislamu. Ina maana kwamba Waislamu lazima wasimame bega kwa bega kulinda maadili ya Uislamu, ardhi ya Waislamu na Umma wa Waislamu.

Lazima wasahau tofauti zao za kimadhehebu wakati wa kukabiliana na Wazayuni, Wamarekani na Wakomunisti. Huu ndio umoja unaopigiwa kampeni na viongozi wa Iran. Haina maana kwamba lazima tufiche imani zetu, bali humaanisha tu kwamba Masunni na Mashia lazima waache kutukanana katika imani na desturi zao wenyewe. Lakini haina maana kwamba tuache kuhubiri fikra zetu miongoni mwa Masunni katika hali ya uwazi na kielimu.

Sio jambo la siri tena kwamba Marekani na marafiki zake wametangaza waziwazi kwamba, "Sasa baada ya kuusambaratisha Ukomunisti adui yetu namba moja aliyebakia ni Uislamu," na madhumuni yao ni kuufuta Uislamu katika ramani ya ulimwengu - kitu ambacho hawatafanikiwa kamwe.

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 3 10/26/2015 1:14:48 PM

Waislamu ni wale wote wenye kuamini mambo yaliyotajwa hapo juu, na maadui wanaelewa hivyo hivyo. Kwa hiyo kwao wao hawaangalii madhehebu. Maadamu wewe unajiita ni Mwislamu basi wewe ni adui wao. Hawaangalii kwamba wewe unatoka katika madhehebu gani. Bali wao huzitumia tu madhehebu na kutuchonganisha ili waweze kutushambulia kwa urahisi. Na hii ndio mbinu kubwa wanayotumia sasa hivi, wametukoroga na tumekorogeka, anaanza na mmoja akishammaliza anamchukuwa mwingine, akishammaliza anamchukuwa mwingine na mwingine mpaka mwisho. Kwa hiyo, wewe usijidanganyike kumuona mwenzako wa madhehebu nyingine akishambuliwa na adui huyu au yule wewe ukashangilia, ujue kwamba atakapommaliza yule atakurudia wewe. Angalia wanavyofanya Afghanistan, Iraq, Lebanon, Palestina, Somalia, Syria na sasa wanataka kuivamia Iran. Waislamu adui yetu ni mmoja, lazima tuwe wamoja ili kumkabili adui yetu huyu aliyejidhihirisha wazi wazi, tuache kutupiana madongo wenyewe kwa wenyewe, tusiwape maadui zetu nafasi ya kutumia hitilafu zetu za madhehebu na kutuchonganisha nazo. Yule ambaye halitaki hili na kuleta visingizio vya hapa na pale na kuzusha fitna, kwa hakika huyo hautakii mema Uislamu na yafaa naye ahesabiwe kama adui wa Uislamu. Hapa lazima ieleweke wazi kwa wale ambao hujihusisha na harakati hizi za kushambuliana kwamba wanaonufaika na mchezo wao huu ni Israil, Marekani na washirika wake wa Magharibi.

Sisi kama wachapishaji tunakiwasilisha kitabu hiki kama kilivyo kwa wasomaji wetu na kuwashauri wasome yaliyomo humo, wayafanyie kazi na kuyazingatia na kufaidika na hazina iliyoko ndani ya kitabu hiki.

Hii ni moja kati ya kazi kubwa zilizofanywa na Taasisi ya Al-Itrah katika kuwahudumia kielimu wasomaji wake wazungumzaji wa Kiswahili. Na kwa maana hiyohiyo imeamua kukichapisha kitabu

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 4 10/26/2015 1:14:48 PM

hiki chenye manufaa makubwa kwa lugha ya Kiswahili kwa lengo lake lilelile la kuwahudumia Waislamu hususan wanaozungumza Kiswahili.

Hivyo, ni matumaini yetu kwamba wasomaji wetu watanufaika vya kutosha kutokana na kitabu hiki, kwani tumekiona ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshahaji wa historia na kugombanishwa wenyewe kwa wenyewe ni vitu ambavyo havina nafasi tena katika akili za watu.

Tunamshukuru mwandishi wa kitabu hiki Sheikh Hasan Musa as-Saffar kwa kazi kubwa aliyofanya kwa ajili ya Umma huu wa Waislamu, Allah Azza wa Jallah amlipe kila la kheri na amuingize Peponi kwa salama na amani insha'Allah. Halikadhalika tunamshukuru ndugu yetu Abdul Karim Juma Nkusui kwa kukitarjumi katika lugha ya Kiswahili kitabu hiki. Insha'Allah Allah Azza wa Jallah amlipe kila kheri hapa duniani na Akhera pia, bila kuwasahau na wale wote waliochangia kwa namna mmoja au nyingine mpaka kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah Mwenye kujazi awalipe wote malipo mema hapa duniani na Akhera pia.

Mchapishaji
Al-Itrah Foundation.

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 5 10/26/2015 1:14:48 PM

بسم الله الرحمن الرحيم

UTANGULIZI

Nilipata mwaliko kutoka katika kitivo cha masomo ya Kiislamu katika chuo kikuu cha Qatar, na kitivo cha sharia na masomo ya Kiislamu katika Taasisi ya Qatar ya malezi na sayansi, ili kushiriki katika kongamano lililofanyika Doha mnamo 12 - 13/ 5/1431 Hijiria, sawa na 25 - 26/4/2010. Kongamano lililokuwa chini ya anwani: **"Kufanya Ijtihadi katika mazungumzo ya Kiislam ili kuelekea kwenye mazungumzo mapya ya kibinadamu"**. Na waratibu wa kongamano wakapendekeza ushiriki wangu uwe katika mada inayohusu **"Kutazama Upya Mazungumzo ya Umoja."** Na huu ndio waraka mdogo niliouwasilisha katika kikao cha tatu cha kongamano, na pakawa na uchangiaji na majadiliano muhimu na mazuri sana wakati wa kikao.

Na miongoni mwa sifa za kongamano hili ni kwamba washiriki walikuwa ni idadi ndogo ya maulamaa na watafiti, miongoni mwao ni Allammah Dr. Sheikh Yusufu al-Qaradhwawiy, bila ya kuwepo wahudhuriaji rasmi au wananchi au wanahabari, jambo ambalo lilitoa fursa ya kupatikana majadiliano ya wazi na ya kina. Na mazungumzo nje ya kongamano yalikuwa na faida kubwa, si chini ya faida ya utafiti na mijadala iliyofanyika ndani ya vikao vya ndani ya kongamano.

Hakika kuna haja sana ya kuwepo makongamano na mikutano ambayo italeta mawasiliano ya kielimu na kijamii baina ya pande na shakhisiya zenye uchungu na umma kwa ajili ya kuendeleza fikra na mikakati, na kuusogeza umma kwenye maendeleo na kuuwezesha

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 6 10/26/2015 1:14:48 PM

kukabiliana na changamoto, na kuulinda na mielekeo ya kasumba, kupetuka na mpasuko.

Na mbele ya wasomaji wapendwa, nauweka waraka ambao niliuwasilisha katika kongamano, nataraji katika kuusambaza kwake kutakuwa na faida kubwa na kuwashirikisha wasomaji katika kujadili yaliyomo humo miongoni mwa fikra. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kuwafikisha.

Hasan Musa as Saffar

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 7 10/26/2015 1:14:48 PM

بسم الله الرحمن الرحيم

MAZUNGUMZO YA UMOJA, UKOSOAJI NA USAHIHISHAJI

Mazungumzo ya umoja leo katika medani ya umma yanakabiliwa na changamoto hatari, na zinazojitokeza zaidi ni hizi zifuatazo:

Kwanza: Sababu ambazo ni hali ya mgawanyiko, siasa za ubaguzi, vita vya ikhitilafu na misukosuko ya fitina. Hiyo ni kwa sababu mfumo wa kisiasa na kijamii katika nchi zetu nyingi za Kiislamu hauwapi wananchi wake fursa ya kuneemeka kwa uadilifu na usawa, kama lilivyo lengo la sharia ya Kiislamu na makusudio ya dhana ya uraia na mikataba ya haki za binadamu.

Kuna ubaguzi baina ya raia katika haki, na nafasi za ushiriki katika utawala na pato, kwa sababu ya tofauti za uhusiano wao wa kiukoo, kikabila, kidini na kimadhehebu. Hali hiyo imesababisha mlipuko na vita vya umwagaji damu katika nchi za Kiislamu, kama ilivyotokea katika Sudani ya Kusini, Darfur magharibi mwa Sudani, Kusini mwa Iraki na Mashariki mwa Uturuki. Na wanalalamika baadhi ya wale walio wachache katika madhehebu, Sunni katika jamii ya Mashia, na Shia katika jamii ya Masunni, kutokana na siasa za ubaguzi, zinazotengeneza mazingira ya fitina na mfarakano na kuzalisha hali za mizozo na mapigano.

Hakika kujitokeza kwa dosari hizi katika sehemu nyingi kunadhoofisha uhalisia wa mazungumzo ya umoja katika medani ya

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 8 10/26/2015 1:14:48 PM

umma, na hatimaye mazungumzo hayo katika mtazamo wa wale wenye kuungua kwa moto wa ubaguzi na kunyimwa haki yanageuka na kuwa ni anwani tu kubwa na nembo nzuri yenye kuvutia (bila ya faida yoyote).

Pili: Kuenea sana mazungumzo ya uchochezi na yenye kusheheni ubaguzi, ambapo sio tu ni khutuba katika msikiti au Husainiya, na sio tu kitabu kilichochapishwa bali ni matangazo yenye kupita hadi kwenye mabara mengine kupitia runinga, chaneli za runinga, tovuti na matumizi ya simu za mikononi. Wazalishaji wa matangazo yenye kusheheni ubaguzi wanashindana katika kuchochea hisia na kuamsha chuki na bughudha, ili kupata sehemu pana zaidi kutoka kwa watu washuhudiaji na wapokeaji, kwa kuchambua matukio ya mzozo wa kimadhehebu katika kina cha historia na kutafuta sehemu za ubaya katika vitabu vya hazina ya zamani, na kuzikuza ili zilete msuguano hapa na pale, bali na kutengeneza uwongo na uzushi ikiwa hawakupata ubaya.

Mazungumzo haya ya ubaguzi yameshakuwa ni sauti ya juu na yenye kupaa, ili kutekenya hisia na dhamira na kuiegemeza katika nyaraka za fitina na uchochezi wenye kuendelea. Na wameweza kuzingira na kuyadhibiti mazungumzo ya umoja na kuamiliana, na kuyazungushia fikra nyingi na maswali, katika sehemu kubwa ya umma, bali athari ya mazungumzo ya ubaguzi imeendelea na kupenya hadi kwenye nafsi za baadhi ya viongozi wa mazungumzo ya umoja, na viongozi wa kati na wenye wastani katika umma, chini ya kisingizio cha upinzani na kulipiza kisasi dhidi ya misimamo ya ubaguzi kutoka upande mwingine. Na hii ni miongoni mwa yanayosikitisha sana, ambapo yanatengeneza hali ya kurudi nyuma yenye kuudhi na kuzuia juhudi za umoja na kukurubiana, na kutoa zawadi bora na chumo kwa walinganiaji wa fitina na mgawanyiko.

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 9 10/26/2015 1:14:48 PM

Tatu: Udhaifu wa kuitikia mazungumzo ya umoja kwa madai ya kuboresha na kuendeleza, mengi miongoni mwa mazungumzo hayo yanakabiliwa na hali ya kudumaa na kunyamaza katika madhumuni yake, na mbinu ambazo yanazitumia, katika kiwango cha harakati na uwezekano wa kuathiri. Na waraka huu mdogo unajaribu kuzindua dharura ya kuboresha na kutazama upya mazungumzo ya umoja kupitia kuhamasisha angalizo na michango zaidi.

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 10 10/26/2015 1:14:48 PM

KATIKA UPANDE WA ASASI ZA KIRAIA

Hakika mazungumzo ya umoja yanakabiliwa na upungufu mkubwa katika upande wa idadi na namna, mukabala wa mamia ya asasi na mimbari za matangazo zinazozalisha uchochezi wa ubaguzi, na zinazosambaza malengo ya kasumba ya kimadhehebu, ambapo hutopata isipokuwa idadi ndogo ya taasisi ndizo zinazojali mazungumzo na mambo ya umoja. Na kati ya makumi ya maelfu miongoni mwa maulamaa wa kidini na wanaojihusisha na masuala ya dini kati ya makhatibu na walinganiaji, ni wachache tu miongoni mwao ndio wenye kubeba jukumu la kueneza umoja na kupambana na utamaduni wa ikhitilafu na mpasuko. Na lau tukichunguza harakati za vitabu na usambazaji wa makala tutakuta kwamba kiashirio cha uzalishaji na usambazaji wa maandishi ya ubaguzi wa kimadhehebu uko juu zaidi ukilinganisha na idadi ndogo ya maandishi yanayolingania umoja na mshikamamo.

Hakika kuna haja sana ya kuwepo taasisi za kiraia zinazoshughulika na kusambaza utamaduni wa umoja na usamehevu na uvumilivu, na kujitolea katika kuzima moto na kuhamasisha mjadala baina ya pande mbalimbali, kwa kuhudumia utulivu na amani ya jamii. Hakika sisi tunakuta katika jamii zilizoendelea maelfu ya taasisi za kiraia zenye kujali mambo ya uhusiano wa kijamii, wakati ambapo sisi tunakosa mfano wa hayo katika jamii zetu.Jumuiya ya *Daru Taqriyb Bainal- Madhaahibil- Islamiyah* imeanzishwa kabla ya zaidi ya nusu karne huko Cairo, kwa juhudi za raia kutoka kwa Marjaa wa kishia na wa kisuni, na ilikuwa ni tajriba yenye kuongoza ambayo ilipokelewa na maulamaa warekebishaji kutoka madhehebu mbalimbali, na likatolewa jarida zuri kwa anwani ya *Risalatul-Islaam*.

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 11 10/26/2015 1:14:48 PM

Yametolewa matoleo sita, tangu mwaka 1368 Hijiria hadi 1392 Hijiria, na lilikuwa ni mimbari ya kuunganisha maulamaa na wanafikra wa umma, wenye kutangaza utamaduni wa umoja na majadiliano, na wenye kulingania mawasiliano na kukurubiana. Lakini taasisi hii haikuweza kuvumilia mbele ya mawimbi ya siasa na wala haikupata msaada wa ulinzi wa kutosha wa raia, shughuli zake zikasimama na harakati zake zikapooza. Na matarajio yalikuwa kusambaza tajriba yake na kuiboresha katika nchi nyingine, lakini hilo halikutokea kwa muda wa miongo miwili hadi ilipoasisiwa Taasisi ya *Majmaul-Alamiy Litaqrib Bainal – Madhaahibil- Islamiyah* katika Jamhuri ya Kiislamu ya Iran.

Katika miongo hii imelipuka mbele ya macho yetu mizozo mikali ya kimakundi katika ulimwengu wa Kiislam, baina ya makundi ya Kiislamu, na yenye kuonekana zaidi ni: Matatizo ya Wakurdi huko Iraki, Uturuki na Iran, na ikaendelea hadi kuwa ni ugomvi wa umwagaji damu, humo wameuliwa makumi ya maelfu, na maelfu wamekimbia, na zimetumika humo silaha za kemikali kama ilivyotokea Halabcha Iraki mwaka 1988, ambapo waliteketezwa raia wa Kikurudi elfu tano wanaume, wanawake na watoto.

Ilikuwa ni aibu kiasi gani, maulamaa na wanafikra na werevu katika umma kuchukua msimamo wa kuangalia tu matukio ya vita hivi au kutosheka kwa kulaani katika kiwango cha mtu binafsi, bila ya kuanzishwa katika umma – pamoja na ukubwa wake - taasisi moja ya kiraia yenye kulingania na kuyaelekeza makundi ya Kiislamu chini ya misingi adilifu na ya usawa.

Na hali ni hiyo hiyo katika mizozo ya kimadhehebu ya kimakundi ambayo wanasiasa walifanikiwa katika uchochezi wake na kuitumia, na wakaipokea wenye akili ya uharibifu kati ya viongozi wa madhehebu wakatoa fatwa za kukufurisha na wakaandika vitabu vya kuchochea chuki. Bali yakaundwa makundi ya wanamgambo

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 12 10/26/2015 1:14:48 PM

ili kumalizana, kama ilivyotokea Pakistani na Iraki, na mambo yakafikia kwenye uadui wa kulipizana katika misikiti, sehemu takatifu na mikusanyiko ya kidini. Yote haya yanatokea, na medani ya umma kukosa juhudi yoyote ya kiraia ya kitaasisi ya kusimama mbele ya fitina hii hatari.

Wakati ambapo medani ya jamii ya kimagharibi, Marekani na Ulaya zimesheheni taasisi nyingi za kiraia ambazo zinashughulika na kusambaza utamaduni wa amani na usalama, na zinakabiliana na mizozo na ugomvi kwa kujitolea kusuluhisha na majadiliano katika viwango vya kiulimwengu, na miongoni mwa taasisi hizo ni: *Karengy international Insitute for peace*, nayo ni taasisi maarufu ya utafiti ya Washington, imeasisiwa tangu mwaka 1910 chini ya uongozi wa Androw Karengy, mmoja wa viongozi muhimu wa viwanda katika muongo huo, ambaye alichuma utajiri mkubwa katika utengenezaji wa chuma, kisha akaamua kujizatiti ili kutimiza malengo yake ambayo alihisi kwamba katika hilo haisihi kutegemea moja kwa moja serikali, bali ni wajibu kuwepo na mashirika maalumu na vyama vyenye kuisaidia serikali katika mambo kadhaa, na moja wapo ni kadhia ya kusambaza amani ulimwenguni.

Liko wapi jukumu la maulamaa wetu, matajiri wetu na jamii yetu katika nyanja za kuanzisha taasisi za kiraia ambazo zinafanya kazi ya kuunganisha safu za umma na kuzima fitina ya mizozo na mifarakano?

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 13 10/26/2015 1:14:48 PM

UWEZO WA KUATHIRI

Katika upande mwingine hakika mazungumzo ya kufarakisha na kutenganisha yanazungumzwa kwa sauti ya juu na kujiamini sana wakati ambapo mazungumzo mengi ya umoja yanasifika kwa kiasi kikubwa kwa aibu na haya. Na huenda miongoni mwa yaliyo muhimu zaidi kuyafahamu katika upande wa ulinganisho baina ya kiwango cha utekelezaji wa wazungumzaji, ni uwezo unaomilikiwa na mazungumzo ya kufarakisha, uwezo wa kuwaathiri watu na kuchochea hisia na hamasa, na kumsukuma mtu kuiendea fitina, vita na ugomvi, wakati ambapo harakati za mazungumzo ya umoja zinakaribia kuishia katika kiwango cha jopo dogo, jambo ambalo linahitajia utafiti zaidi katika kujenga mazungumzo ya umoja, na mbinu za kuzungumza pamoja na watu wa umma, upeo wa uwezo wake katika kuathiri hisia nzuri na hisia za kujenga ndani ya nafsi za watu wa umma kwa ajili ya mafanikio ya mwelekeo wa umoja na misimamo ya amani na uelewano.

Na mtafiti Sheikh Haidar Hubullahi alijiuliza kuhusu tofauti hii, kwa kusema: Kwa nini sauti ya ikhitilafu na mizozo ya ndani inafaulu katika kuchochea jamii yote kwa muda mfupi, wakati sauti ya kuleta ukuruba inahitaji muda mrefu ili kufaulu katika kufanikisha hatua moja tu? Na jibu lake lilikuwa: “Hakika moja ya sababu za msingi katika hilo ni kitendo cha kundi la ikhitilafu kumiliki msaada mkubwa wa kihistoria, hudhihiri kumbukumbu za pamoja kutoka katika kina cha uelewa wa watu, na haraka mno kumbukumbu hizi huathiri kwa kuzalisha picha iliyojaa matukio yenye kuchemka, yenye tabia ya ghadhabu. Ama kundi la kuleta ukuruba lenyewe halimiliki msaada wa kihistoria wala mbinu za kimkakati za kurithi au kwa uchache turathi yenye kusomwa…...”[1]

[1] Haidar Hubullahi: *Mas’alatu al-Manhaji fiyl- fikiri diyn*, chapa ya kwanza 2007, (Beirut Daru al-Intishaarati al-Arabiy) Uk. 50.

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 14 10/26/2015 1:14:48 PM

Pamoja na nafasi ya sababu zilizotajwa, kwa kuongezea ule mchango wa sababu za hali isiyo sawasawa ambayo umma unaishi nayo, ni pamoja na yale inayoyazalisha miongoni mwa matukio ya kisiasa na kijamii, ambayo yanatumikia kundi la ikhitilafu, isipokuwa ni kwamba hayo hayapingi ukweli tunaoushuhudia wa uwepo wa uchupaji ada na uzembe kwa walinganiaji wa umoja katika kuzalisha mazungumzo yenye uwezo wa kuathiri watu wa umma, na kuandaa mkakati unaokubali kukubalika na kuathiri.

Kumbukumbu ya Waarabu wa Bara Arabu ilikuwa imejaa hazina kubwa ya picha za vita na mapigano baina yao kabla ya Uislamu. Na mapigano yaliyokuwa yanatokea mara kwa mara yalikuwa yakidumisha picha hizo katika fikra zao, na kaswida za washairi wao zilikuwa zikihuisha matukio hayo, ambapo zilikuwa zikionesha fahari na utukufu kwa mshindi, na fedheha na aibu kwa upande wa pili, na zikionya na kutishia kulipiza kisasi, na hayo ndiyo yaliyokuwa maudhui ya msingi katika fasihi ya ujahilia.

Lakini mazungumzo ya ujumbe wa Uislamu yalizima harakati za ukumbusho huo wa kijahilia, na yakatengeneza kwa watu uelewa mpya, yakawanyanyua kutoka kwenye mpasuko na uadui kwenda kwenye kilele cha udugu na uelewano, nayo ni neema ya Mwenyezi Mungu ambayo Mwenyezi Mungu amewaneemesha Waislamu, anasema (swt):

وَاذْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ كُنْتُمْ أَعْدَاءً فَأَلَّفَ بَيْنَ قُلُوبِكُمْ فَأَصْبَحْتُمْ بِنِعْمَتِهِ إِخْوَانًا

“Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu juu yenu mlipokuwa maadui naye akaziunganisha nyoyo zenu; hivyo kwa neema yake mkawa ndugu.” (Sura Imraan: 103).

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 15 10/26/2015 1:14:48 PM

Na mbele yetu kuna mfano wa leo, nao ni mwitikio wa wananchi wa Ulaya mbele ya wito wa kuleta ukuruba na muungano, pamoja na kwamba kumbukumbu ya machungu na mapigano ya ndani baina yao bado yangali yanaonekana. Ni ipi rejea ya uelewa wa umoja kwa watu wa Ulaya? Na ni zipi sababu za kuathiri na kukinaisha katika mazungumzo yao ya umoja? Na kwa nini bado hayajafika kwetu mazungumzo ya umoja katika kiwango kinachofaa cha uwezo wa kuathiri? Ni wazi kwamba maamuzi ya muungano wa Ulaya yanawakilisha matakwa ya wananchi na sio matakwa ya kisiasa tu, kwa sababu serikali ambazo zilipitisha muungano na umoja huo zimechaguliwa na wananchi wake, kama ambavyo yalitimia majadiliano yake kwanza katika bunge linalowakilisha wananchi na kura zimepigwa katika baadhi ya nchi hizo.

Hakika ni lazima kuwepo na ujasiri katika kukosoa mazungumzo yetu ya umoja na kuyasahihisha, kwa ajili ya kunyanyuka kwenda kwenye kiwango cha umoja na ili yatekeleze jukumu lake linalotakiwa katika nyanja ya umma. Na tunaposema tunahitaji kufanya ukosoaji wa mazungumzo haya na kuyaboresha, haimaanishi kuwa tunapinga nafasi nzuri ya mazungumzo yaliyotangulia na athari yake muhimu katika historia yetu ya kileo. Mazungumzo haya yamechangia kudumu dhana na msingi wa Kiislamu, na kubakisha uelewa na matarajio haya hai katika uwepo wa utamaduni wa umma, na mazungumzo ya umoja yalikuwa na juhudi za mawasiliano na ukuruba zilizotolewa, dauru ya kuweka mpaka katika kukabiliana na kasumba na mpasuko, na kupunguza hasara na madhara.

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 16 10/26/2015 1:14:49 PM

KUKUBALI WINGI WA MADHEHEBU

Mazungumzo ya umoja yamejikita katika kudhihirisha upana wa maafikiano baina ya madhehebu na makundi ya Kiislamu, na kupunguza jambo la ikhitilafu, na kutia mkazo kwa kila yanayodhihirisha mfanano na maafikiano baina yake katika nyanja ya kiitikadi na kifiqihi. Na hapana shaka kwamba mapendekezo haya yanaanzia kwenye msingi sahihi na yanategemea ukweli uliopo kwamba wigo wa maafikiano ni mpana zaidi kuliko sehemu za ikhitilafu.

Kama ambavyo mapendekezo haya yanalenga kukabiliana na hali ya kukuza na kutia chumvi ambako kunafanywa na pande za madhehebu yenye kushadidia, ambazo zinafanya ikhitilafu hizo chache kana kwamba ndio ubainifu tosha unaogawa umma pande mbili na kudhihirisha madhehebu mengine kama dini nyingine. Imechapishwa – kwa mfano – kabla ya miongo kadhaa kitabu mashuhuri sana chini ya anwani *al-Khututwul-Ariydhwa Lil'ususi Alatiy Qaama Bihaa Diyn Shia'ah*, na kikapingwa na kitabu kingine chini ya anwani *al-Khututwu Twawilatu Lil'ususi Alatiy Qaama Bihaa Diyn Sunnah*. Huku kukuza na kutia chumvi katika mambo ya ikhitilafu za kimadhehebu ndio ambako kumesukuma mazungumzo ya umoja ili kuimarisha hali ya maafikiano na maelewano na kupunguza jambo la ikhitilafu baina ya madhehebu ya Kiislamu.

Lakini kuna tahadhari ambayo ni wajibu tutanabahi kwayo, nayo ni kwamba mazungumzo haya yanaweza kukuza ikhitilafu, hivyo inapasa kwenda mbio kuistiri na kuificha kadri iwezekanavyo. Kama ambavyo mfumo huu unaweza kuficha mafungamano ya umoja uliyopo katika mambo ya kidini na kifiqihi. Kuna udhaifu usiofichikana ndani ya baadhi ya madhehebu katika uelewa wao juu ya umoja na ukuruba, jambo linaloweza kuwafanya watoe wito wa

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 17 10/26/2015 1:14:49 PM

kuutaka upande huu au ule uachane na baadhi ya itikadi zake na sifa zake mahususi, na hivyo watu hawa wanakabiliwa na changamoto ya kutaka kuudhihirishia umma katika mandhari moja na muundo mmoja katika fikra na mwenendo kwa madhehebu nyingine kumezwa na madhehebu moja.

Na ukweli ni kwamba haiwezekani kupinga uwepo wa ikhitilafu za kimsingi katika mambo ya kiitikadi na kifiqihi baina ya madhehebu na makundi ya Kiislamu, pamoja na kuafikiana katika misingi ya imani na nguzo za Kiislamu. Na ikhitilafu hii sio kosa wala si aibu, bali ni matokeo ya kawaida kwa ajili ya kutumia ijitihadi na kutazama nususi za kisharia ambazo zinaweza kuwa na zaidi ya maana na tafsiri moja. Na nyingi kati ya hizo zinatokana na ikhtilafu za watu wa zama za mwanzo za Uislamu, wale wa mwanzo katika umma ambao madhehebu haya yanajinasibisha kwao.

Na inafahamika kwamba ikhitilafu za ijitihadi zimezalisha utajiri katika maarifa ya umma, na zimeimarisha uhuru wa rai na fikra, na zimetoa chaguo nyingi katika kutatua baadhi ya matatizo ya kifikra na ya kimaisha ambayo yanaukabili umma. Lakini tatizo la umma, muamala na uhusiano mbaya pamoja na rai nyingine, baina ya pande zinazokhitalifiana kwa kuanzia na kupinga haki yake katika uwepo na kumalizia na kufuta uhai wa anayesema hivyo, au kukata dauru yake au kuipuuza, na kumbana na kumnyamazisha.

Hapana shaka kwamba ufahamu huu wa umoja ni kosa linalopingwa, umoja haulazimishi kufuta uhuru wa kufikiria, uhalali wa ijitihadi, wala haumaanishi kulazimisha rai kwa nguvu kwa watu, kwa sababu hilo linakhalifu tabia ya kibinadamu iliyopo katika kutofautiana, na tabia ya nususi za kidini, nasi yoyote ya kunukuu inakubali kujadiliwa kuhusu usahihi wa nukuu yake isipokuwa nasi ya Qur'ani ambayo hakuna shaka juu ya nukuu yake. Au kufaha-

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 18 10/26/2015 1:14:49 PM

mu makusudio yake jambo ambalo pia linaihusu nasi ya Qur'ani na nususi za Sunnah tukufu na kauli za Maimamu na mafaqihi.

Kama ambavyo kulazimisha rai kunapingana na dhahiri ya nususi za kidini ambazo zinatia mkazo juu ya utukufu wa mwanadamu na kuheshimu haki yake katika kufikiri, kuchagua na kutoa rai. Tunakuta katika sira ya watangulizi wa umma rai nyingi na ijitihadi za kiitikadi na za kifiqihi baina yao, nayo ni hali ya tangu zamani na kongwe katika historia ya umma, na maimamu na mafaqihi wanaendesha tofauti zao katika medani ya utafiti na majadiliano kupitia zana za hoja na dalili. Na kuvuka duara hili na kwenda kwenye mzozo na ugomvi aghlabu ilikuwa inatimia kwa sababu za kisiasa na msukumo wa kimaslahi.

Na katika sira ya Amirul-Muuminina Ali bin Abi Twalib عليه السلام kuna kigezo na mfano bora, ambapo hakukabili rai za Makhawariji za kiitikadi na kisiasa kwa ukandamizaji na mabavu, na wala hakupokonya chochote katika haki zao za kidini kwa sababu yake, bali alitangaza dhamana kwao maadamu hawajavuka mpaka wa rai na kuchomoa silaha na kuchochea fitina.

Imekuja katika *Tarikh Twabariy* kutoka kwa al-Hadhwaramiy amesema: "Siku moja Ali alisimama mbele ya watu akiwahutubia, mtu mmoja kutoka upande wa msikiti akasema: 'Hakuna hukumu isipokuwa ya Mwenyezi Mungu.' Na mwingine akasema mfano hayo, kisha wakafuatia wengine wakisema hakuna hukumu isipokuwa ya Mwenyezi Mungu. Ali akasema: 'Allahu Akbar, neno la haki lakini limekusudiwa batili, ama hakika nyinyi mnayo kwetu mambo matatu maadamu mtasuhubiana nasi: Hatuwakatazi misikiti ya Mwenyezi Mungu kutaja humo jina lake, wala hatuwazuii pato maadamu mikono yenu ipo pamoja na mikono yetu, wala hatuwapigi vita hadi nyinyi mtuanze.' Ki-

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 19 10/26/2015 1:14:49 PM

sha akarejea na akaendelea na khutuba yake.[2] Na katika *Tarikh Twabariy*, kutoka kwa Abdul-Malik bin Abiy Hurrah al-Hanafiy amesema: "Hakika siku moja Ali alitoka na kuhutubia, mara akiwa katika khutuba yake mtu mmoja kutoka upande wa msikiti akasema: 'Hakuna hukumu isipokuwa ya Mwenyezi Mungu.' Ali akasema: 'Allahu Akbar, neno la haki lakini limekusudiwa batili, kama watanyamaza tutawajumuisha, na kama watazungumza tutajadiliana nao kwa hoja, na kama watatoka dhidi yetu tutawapiga vita.'"[3]

Na baada ya vita ya Nahrawan baadhi ya wafuasi wa Ali walimsikia mtu anayeitwa Abu al-Izaari Twaiy akitangaza rai ya Makhawariji. Wakamleta kwa Imam Ali wakisema: Hakika huyu anatangaza rai ya Makhawariji na ananukuu maneno yao, akasema عليه السلام: "Nimfanye nini?"

Wakasema: Muuwe. Akasema: "Nimuuwe mtu asiyenipiga vita?"

Wakasema: Basi mfunge jela. Akasema: "Hana kosa la kumpeleka kifungoni, mwacheni huru."[4] Kama ambavyo Amirul-Muuminina hakutumia ukandamizaji wa kisiasa dhidi ya mahasimu wake, hakika hakutumia ugaidi wa kifikra dhidi yao, hakuwakufurisha au kushuku katika dini yao.

Katika *Kanzul-Ummaal* kutoka kwa Abi al-Bahtariy amesema: "Ali aliulizwa kuhusu watu wa Jamali, pakasemwa: Je, wao ni washirikina? Akasema: 'Kwenye ushirikina walishakimbia.' Pakasemwa: Wao ni wanafiki? Akasema: 'Hakika wanafiki hawamtaji

[2] Muhammad bin Jariri Twabariy katika Tarikh Juz. 4, chapa ya tano 1409 Hijiria, (Beirut Muasasatu al-alamiy lilimatubuaati) Uk. 53 na vilevile katika Sunanul-Kubra ya al-Baihaqiy, Juz. 8, Uk. 184.

[3] *Tarikh Twabariy* Juz. 4 uk: 53.

[4] *Al-Khatwib al-Baghidadiy* Juz. 14 (Beirut Darul- kutubi al-ilimiya) Uk. 366

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 20 10/26/2015 1:14:49 PM

Mwenyezi Mungu isipokuwa kidogo tu.' Pakasemwa wao ni nani? Akasema: 'Ni ndugu zetu waliotuasi.'"[5]

Amepokea al-Baihaqiy na Ibnu Abdi al-Barri katika *Jami'u Bayaanil-Ilmi* kutoka kwa khalifa Abdul-Aziz kwamba amesema: "Kinachonifurahisha mimi ni kwamba masahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu pamoja na hayo, hawakuzozana, kwa sababu hakika wao kama wasingelikhitalifiana basi tusingekuwa na ruhusa."[6]

Amesema Dr. Sheikh Yusuf al-Qaradhwawiy: "Yaani hakika wao kwa ikhitilafu yao wametupa fursa ya kuchagua baina ya kauli zao na ijitihadi zao kama ambavyo hakika wao wameanzisha tafauti katika mambo ya ijitihadi."[7] Na alipotaka khalifa wa Ban Abbas Abu Ja'far al-Mansur kuwalazimisha watu kufuata rai ya Imam Maliki kwa kumwambia: "Nimeazimia kutoa amri juu ya vitabu vyako hivi ambavyo umevitunga, vitolewe nakala kisha nitume katika kila mji kati ya miji ya Waislam nakala moja na niwaamuru wafanyie kazi yaliyomo humo wala wasivuke kwa kufanyia kazi kitabu kingine." Imam Maliki alisema: "Ewe Amirul-Muuminina usifanye hivyo, hakika watu zimeshawatangulia kauli na wamesikia hadithi na wamepokea riwaya na kila watu wakachukua yaliyotangulia kwao, na wakaleta tafauti za watu, waache watu na walichochagua watu wa kila mji miongoni mwao kwa ajili ya nafsi zao."[8]

Hakika kuwa na madhehebu mengi na kutofautiana rai ni jambo lipo katika historia ya umma na katika hali yake ya leo, na hakuna

[5] Alau Diyn Ali al-Mutaqiy bin Hasaam al-Hindiy katika *Kanzul-Umaal*, Juz. 11, Chapa ya tano 1405 Hijiria (Beirut Muasasatu Risalah) Uk. 335.

[6] Amepokea al-Baihaqiy katika *al-Madikhali Fiy Faidh al-Qadir*, Juz. 209 na Ibnu Abdial-Barr katika *Jaami'u Bayaanil- ilimi,* Juz. 2, Uk. 80, Chapa ya al- Maniriyah.

[7] Yusufu al-Qaradhwawiy katika *As-Swahawatul-Islamiyah Baina al-Ikhitilafu al-Mashuru'u wal-Firaqi al-Madhumum*, Chapa ya tatu, 1414 Hijiria (Beirut muasasatu risala), Uk. 49.

[8] *Hujjatullahi al-Baalighah*, Juz. 1 uk: 145 chapa ya Misri 1352 Hijiria.

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 21 10/26/2015 1:14:49 PM

budi ya kulitambua, na kuamiliana nalo na hususan katika zama hii ambayo humo kunapatikana uwezekano na fursa katika pande mbalimbali, hakuna badili ya kuitambua na kuheshimiana isipokuwa tufani ya fitina, na mateso ya ugomvi na mpasuko, na kushughulika na mizozo ya ndani kwa gharama ya maslahi ya umma na kujenga nchi.

Pamoja na kwamba kuna anayeugawanya wingi wa madhehebu sehemu mbili: Wingi unaokubalika, nao ni ule utokanao na tafauti ya madhehebu katika yale yanayofungamana na mas'ala ya kifiqihi, kulingana na misingi ya uchambuzi na ijitihadi na katika kiwango cha rai ya kifiqihi.

Na wingi unaokataliwa, nao ni ule utokanao na tafauti ya madhehebu katika mas'ala ya kiitikadi katika matawi na ufafanuzi wa imani, au misingi yenyewe, ambayo ni kumwamini Mwenyezi Mungu, malaika wake, mitume wake na siku ya mwisho. Na hakika – hakuna shaka – hiyo ndio misingi ya Uislamu wa mwanadamu, hawi mwislamu anayepinga moja kati ya haya. Lakini ufafanuzi wa itikadi unaofungamana na moja kati ya misingi hii na matawi yanayotokana nayo, hakika baadhi yake ilikuwa ni mahala pa mjadala tangu zama za makhalifa waongofu, kama vile mazungumzo kuhusu mas'ala ya majaliwa na makadara, na hukumu ya mwenye kufanya madhambi makubwa, na anayefaa kwa uimam na ukhalifa baada ya Nabii ﷺ, na ubora baina ya masahaba na mfano wa hayo. Na yaliyochochewa katika zama zilizofuatia mfano wa mas'ala ya kuumbwa kwa Qur'ani, sifa za Mwenyezi Mungu na mengineyo, ambayo yamenyambuliwa na utafiti ukapanuka humo, na ukageuka kuwa ni makundi na mirengo yenye anuwani maarufu katika vitabu vya madhehebu na makundi, elimu ya theiolojia na falsafa kama vile makundi ya Jabriyah na Mu'utazilah, Marjiah na Maturudiyah, Ashairah na Shiah, Sufi, Salafi na Ibaadhi.

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 22 10/26/2015 1:14:49 PM

Ikiwa baadhi ya makundi na madhehebu hayo ya kiitikadi anwani zake zimeisha na kutoweka, hakika watu wa umma wa leo wamegawanyika katika makundi matano ya kiitikadi yenye kuonekana nayo ni: al-Ashairah, as-Sufiyah, Shiah, as-Salafiyah na Ibaadhiyah. Na zimetofautiana rai katika baadhi ya ufafanuzi wa kiitikadi ndani ya makundi haya yenyewe. Hakika tahadhari na kusitasita katika kukubali wingi wa kiitikadi hauna kisingizio, kwani sababu zile zile zilizozalisha tafauti katika mas'ala ya kifiqihi ndio zile zile zilizosababisha tafauti katika mas'ala ya kiitikadi.

Ama kuhusu hali ya wingi wa madhehebu ya kiitikadi na kifiqihi hakuna hiyari isipokuwa kuamiliana na hali hii kwa uzuri unaokinga umma na shari ya mpasuko na fitina na kupiga hatua katika njia ya umoja na uelewano, na kuusaidia katika kukabiliana na changamoto kubwa. Hakika upande wowote ule hauna haki ya kuhukumu na kumtoa mpinzani wake katika duara la Uislamu, maadamu wanakiri misingi ya imani, nguzo za Uislamu na wanaswali kuelekea katika nyumba tukufu (*al-Ka'aba*). Kama ambavyo yeye anaamini kuwa yuko katika haki na rai yake ni sahihi, na wenzake ndivyo wanavyoamini juu ya rai zao na imani zao.

Na kauli ya kuhukumiana kwa Kitabu na Sunna inaturejesha kwenye mraba ule ule wa kwanza, kwani wote wanakiri kuwa wanarejea katika Kitabu na Sunnah, lakini wanatofautiana katika kufahamu makusudio ya nasi, au kukubali usahihi wa upokezi wa nasi katika Sunna. Na inafahamika kwamba uwepo wa Kitabu na Sunnah haukumaliza hitilafu baina ya umma katika zama zilizopita.

Na kwa wale ambao wanajihadhari hivi sasa kukubali wingi wa itikadi wakumbuke kwamba wingi wa idadi ya makundi ya kifiqihi ambayo wanayakubali hivi sasa yalikuwa yanakataliwa ndani ya wengi katika zama zilizopita, na kulikuwa na kizuizi cha kuyatambua, inashabihiana na kizuizi cha sasa hivi dhidi ya wingi wa iti-

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 23 10/26/2015 1:14:49 PM

kadi, ambapo vitabu vya historia na hazina za kifiqihi zinanukuu baadhi ya fatwa za mzozo na kasumba ya kimadhehebu baina ya Ahlus Sunnah kiasi cha baadhi kuwashusha baadhi yao katika nafasi ya wafuasi wa dini nyingine za Ahlul-Kitabi, kama inavyonukuliwa kutoka kwa Kadhi wa Damascus al-Hanafiy Muhammad bin Musa al-Balasaghuniy aliyefariki mwaka 506 Hijiria, kauli yake: "Lau kama ningekuwa na mamlaka basi ningechukua kodi kwa wafuasi wa Shafi."[9] Na kauli ya mwanachuoni mwingine wa fiqihi: "Haijuzu kumuoza mfuasi wa madhehebu ya Shafi mwanamke wa Kihanafi, kama ambavyo haijuzu kumuoza Ahlul-kitabi mwanamke wa Kiislamu."[10]

Na kuna fatwa za kutosihi swala ya jamaa nyuma ya imam wa madhehebu mengine ndani ya madhehebu ya kisuni, hadi wakati wa karibuni ilikuwa zinasimamishwa katika msikiti mtukufu wa Makka jamaa nne katika kila swala ya faradhi kwa madhehebu manne kabla ya kuunganishwa kwa maamuzi ya mfalme Abdul-Aziz Aali Suudi mwaka 1345 Hijiria yaani miaka 86 iliyopita. Na vimetungwa vitabu katika ufafanuzi baina ya madhehebu ya Kisunni kama vile kitabu cha Imam al-Haramain Abi al-Maaliy al-Jauziy as-Shafiiy *Mughithul- Khaliq Fiy Tarjihi Madhhabil-Haq*, ambaye humo ameyatusi Madhehebu ya Abi Hanifah kwa namna mbaya kabisa."[11] Kama ambavyo Abdillahi bin Ahmad bin Hanbali ameweka fasili takriban kurasa hamsini katika kitabu chake *as-Sunnah* kwa kumsema vibaya Imam Abi Hanifah na madhehebu yake.[12] Na imetokea fitina na

[9] Ibnu Kathiyr Adimishiqiy katika al-Bidayatu Wan-Nihaayah, Juz.12, Chapa ya kwanza 1421 Hijiria (Beirut Darul-kutubi al- ilimiyah) Uk. 191.

[10] Muhammad Naaswir al-Albaaniy katika Swafatu Swalati Nabiyyi mina Takibiri ilaa Tasliimu Taannaka Taraha, Chapa ya sita 1391 Hijiria (Beirut al- maktabil- Islaami), Uk. 50.

[11] Muhammad Idd Abbasi katika Bida'atu Ta'asub, Chapa ya pili 1406 Hijiria, (Amaan Maktabatu al-Islamiyah), Uk. 207.

[12] Muhammad Idd Abbasi katika Bida'atu Ta'asub, Chapa ya pili 1406 Hijiria, (Amaan Maktabatu al-Islamiyah), Uk. 207.

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 24 10/26/2015 1:14:49 PM

mzozo baina ya madhehebu ya Ahlus-Sunnah uliosababisha vita na uharibifu katika nchi, matukio yake yameandikwa na vitabu vya historia lakini umma umeshavuka hali hiyo katika nyanja ya uhusiano baina ya madhehebu manne ya Ahlus-Sunnah na mahala pake pakachukuliwa na uhusiano, heshima na uelewano. –Je, tunahitaji karne zingine za ugomvi ili tukubali madhehebu ya itikadi kama ilivyotuchukua karne nyingi kukubali madhehebu ya kifiqihi?

Tunayotaka kuyafikia ni dharura ya kutia mkazo mazungumzo ya umoja, kwamba umoja haumaainishi kufanana na kulingana katika ufafanuzi wa itikadi, na kwamba ni juu ya Waislamu hawa wawakubali wenzao kama walivyo bila kujali tofauti za kiitikadi ndani ya uzio wa Uislamu ambao unawakilishwa katika misingi ya imani na nguzo za Kiislamu. Na unabaki wazi mlango wa majadiliano ya kisharia na nyanja za utafiti wa kielimu kwa maulamaa, kwa kuwasilisha baadhi ya rai zao za kiitikadi kwa lugha ya hoja na dalili, kama hali ilivyo katika upande wa masomo na utafiti wa kifiqihi, ambapo zimetoka rejea za kifiqihi zinazobeba mitazamo ya madhehebu nane za kifikiqihi, na zimeandikwa na kongamano la Kiislamu la *Majmau Lifiqihil-Islamiy*, lenye vikao vyake vilivyopangika ambavyo humo wanajadili wanachuoni wa fiqihi wa Kiislamu kwa madhehebu zao mbalimbali mambo yaliyopendekezwa kujadiliwa na kufanyiwa utafiti.

Imebakia kusawazisha uhusiano katika upande wa ikhitilafu za kiitikadi baina ya pande za umma wa Kiislamu, kati ya Ashairah, Salafiyah, Sufiyah, Ja'fariyah, Zaidiyah na Ibaadhi. Na makusudio ya kusawazisha uhusiano sio kuuzuia kila upande kukiri usahihi wa rai ya upande mwingine, na wala si kuondoa upinzani wake dhidi yake, bali makusudio ni kuhamisha ikhitilafu katika medani ya imani na fikra kwenda kwenye uwiano wa usahihi na kosa, kwani mwenye kukhalifu katika ufafanuzi wa kiitikadi sio kafiri wala sio

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 25 10/26/2015 1:14:49 PM

mwanabidaa (mzushi), bali ni mwislamu aliyekosea katika rai yake na ijitihadi yake, na wala haadhibiwi kwa matokeo ya lazima ya kauli yake, matokeo ambayo hayaamini wala kushikamana nayo. Na hapo inajitokeza dharura ya kujuana baina ya makundi ya kiitikadi kwa kusoma itikadi za kila upande kutoka katika rejea wanazoziitakidi kwa sasa katika nyanja za kiitikadi, ndani ya rai mashuhuri katika nyanja yake, na sio kupitia mkusanyiko wa hadithi au vitabu vyake vya kihistoria au ambayo yanaelezea rai binafsi zenye kutoka nje ya jamii yake.

Hakika cha muhimu na cha msingi katika mazungumzo ya umoja katika zama hizi ni kukinaisha medani ya umma, kusimamisha mashambulizi ya uchochezi, na kudhihirisha ubaya kwa vielelezo na vitu vitakatifu baina ya madhehebu ya kiitikadi, na kutegemea lugha ya uwasilishaji wa kimaudhui, na majadiliano ya kielimu. Hiyo ndio njia ambayo italeta matumaini kwa kila upande kwa uhalisia na ukweli wa kulingania umoja, na kwamba haimaanishi kukiri kosa kama ambavyo haimaanishi ubabe na kulazimisha wala mzozo na ugomvi.

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 26 10/26/2015 1:14:49 PM

KUJENGEA DHANA MPYA

Lengo la msingi la mazungumzo ya umoja ni kusahihisha uhusiano baina ya makundi na pande za jamii ya Kiislamu, na kuihami kutokana na mizozo na mpasuko, ili iishi kwa utulivu na amani ya ndani, na kuelekea katika maendeleo na kujenga, na kutumikia maslahi makuu na kukabiliana na changamoto hatari. Mabadiliko ya kimaisha ya binadamu katika zama hizi yameibua dhana mpya, tunaweza kufaidika nayo katika kutimiza lengo hilo linalotakiwa, ambapo dhana hizo zinatufupishia njia ya kulifikia.

Na miongoni mwa dhana hizo ni dhana ya URAIA na dhana ya HAKI ZA BINADAMU, kwani imejitokeza dhana ya Uraia na istilahi ya Uraia baada ya mapinduzi ya Ufaransa, nayo ni dhana inayofungamana na jiografia, yaani kwa udongo wa ardhi wanaoshirikiana humo kundi la watu, katika kivuli cha dola inayowawakilisha, na kupanga haki na wajibu baina yao, kwa misingi ya kanuni na sharia, mbali na tofauti na sifa mahususi za kiukoo na kidini. Na kwa kuanzia na dhana hii imeasisiwa dola ya kisasa huko Ulaya kwa kufutilia mbali dola ya kanisa, na ikaenea katika ulimwengu mfano wa dola hii, na baada ya kuanguka ukhalifa wa Uthmaniya katika ulimwengu wa Kiislamu, mwanzoni mwa karne ya ishirini, hali ikaelekea katika kusimama dola za nchi, baada ya msaada wa wakoloni wa kudhibiti na kuchora ramani ya mipaka ya jografia katika nchi nyingi za Kiarabu na za Kiislamu. Kila Mwislamu hivi sasa ananasibiana na nchi yenye mipaka ya kijografia, na serikali yenye kutawala, na katika nyingi ya nchi hizi kuna mchanganyiko mbalimbali wa kiukoo na kikabila, kidini na kimadhehebu.

Hakika kutimia dhana ya uraia katika kila nchi kati ya nchi za Kiislamu inamaanisha kuwepo kwa uongozi wa kanuni, usawa baina

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 27 10/26/2015 1:14:49 PM

ya wananchi katika haki na wajibu, na kushiriki kwao katika kuendesha mambo ya nchi yao, kama hali ilivyo katika nchi zilizoendelea. Na hayo ndio mambo yanayotengeneza mazingira ya umoja na kuleta amani na utulivu katika nchi. Hakika miongoni mwa sababu muhimu sana za mizozo na ikhitilafu katika baadhi ya nchi za Kiislamu ni kutokuwepo na ushirikishwaji wa wananchi na kuwepo siasa ya ubaguzi, ukabila na za kimakundi, na kundi fulani la wananchi linapohisi kupuuzwa, kunyimwa na kupunjwa haki zao huku kukitengenezwa kundi jingine katika nafasi ya upendeleo na kutukuzwa, hakika hilo linasababisha mzozo na mapigano ya haraka au ya baadaye.

Hakika nchi nyingi za Kiarabu na za Kiislamu zinakabiliwa na matatizo ya ndani katika muundo wake, hali ambayo inatishia umoja wake na utulivu wake, na kukwaza ustawi na maendeleo, na kufungua mlango mbele ya matakwa na tamaa za nje. Na mas'ala ya ubaguzi yamekuwa ni kati ya anwani dhahiri ya mzozo na mpasuko, na mianya ya fitina katika hali ya umma wa kileo, na ili kutatua mas'ala ya ubaguzi katika nchi yoyote ni wajibu kuanza na utulivu na usawa baina ya wananchi na kuondoa tofauti zozote za ubaguzi, na hii ndio maana inayomaanishwa na dhana ya Uraia, kwa dola kuangalia wananchi wake kama raia kabla ya kitu chochote, na kwa kufumbia macho anwani nyingine za pembezoni. Sambamba na dhana ya Uraia kuna dhana ya Haki za Binadamu, ambayo inamaanisha kuheshimu ahadi na mikataba ya kimataifa ambayo inazungumzia suala la binadamu wote kuneemeka na haki zote za ubinadamu na uhuru uliopo, na miongoni mwayo ni haki ya kuishi, uhuru, usawa, uhuru wa kufikiri, itikadi na kutoa rai.

Hakika kitendo cha serikali kuheshimu na kushikamana na mikataba hii ya kimataifa na watu kujilazimisha kuheshimu mikataba hii mbele ya wenzao, kunatengeneza mazingira ya amani na utulivu,

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 28 10/26/2015 1:14:49 PM

na watu kupata matumaini katika uhusiano wao baina yao, na hivyo wanakuwa ni wenye kuweza kusaidiana na kuwa karibu na umoja. Hakika hali nyingi za uadui na ubaya wa kutendeana baina ya wafuasi wa madhehebu unawakilishwa na mwonekano dhahiri wa uvunjifu wa haki za binadamu, kama vile kupora uhuru wa kidini, kiutamaduni wa madhehebu fulani au vitendo vya ubaguzi dhidi yao kwa sababu tu ya uhusiano wao wa kimadhehebu.

Hivyo ni wajibu mazungumzo ya umoja kujenga dhana hizi mpya, ambazo zinaafikiana na misingi ya dini na makusudio ya sharia, na kutoa nafasi mbele ya hatua ya ukuruba na ufahamu sahihi juu ya umoja. Kama ambavyo ni kuwakilisha lugha ya ulimwengu anayoifahamu mwanadamu wa zama hizi, na ambayo inaungwa mkono na asasi za kimataifa na mazingira ya kiulimwengu.

Na kuwa kwake ni jambo geni katika kanuni, haimaanishi kwamba ni geni kama dhana katika misingi ya Kiislamu na mafunzo yake, kwani kuna maulamaa kadhaa wa Kiislamu na wanafikra wake ambao wameshawasilisha utafiti wa asili ya dhana hizi katika uongofu wa Kiislamu na sharia zake pamoja na kuashiria katika baadhi ya sehemu za kujihadhari na zenye ikhitilafu. Na hakuna katika dini yetu jambo ambalo linazuia kunufaika na uzoefu wa jamii za kibinadamu na matokeo ya mabadiliko ya maisha, hekima ni mali ya muumini iliyopotea anaichukua popote anapoikuta.

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 29 10/26/2015 1:14:49 PM

KUPANGA MSIMAMO

Mtu yeyote au upande wowote hausiti katika kuzungumzia msingi wa umoja na dharura yake kisharia na kiakili, na katika kulaumu mfarakano na mzozo na madhara yake katika dini na maisha. Na katika kiwango hiki cha ujumla inakaribia kutokuwa na tofauti ya mazungumzo ya dini na mengine, na wala huwezi kutenganisha baina ya mazungumzo ya umoja na mengine ya mpasuko. Lakini tatizo linaweza kutokea baada ya anwani hii ya kupanga dhana ya umoja na dhana ya kuitimiza kwake, na ukweli wa uhalisia katika utekelezaji wake. Lakini kila unapokaribia kupanga misimamo ya kivitendo katika uhalisia unakabiliwa na vikwazo na vizingiti, vinavyoonekana katika masharti na vizuizi vinavyotokana na hali ya uwiano wa kisiasa na kijamii uliopo.

Na haya ni katika mambo ambayo yanaonekana katika mazungumzo ya umoja kwa daraja tofauti, ambapo baadhi wanakosa ujasiri na uwazi katika kupanga misimamo ya kivitendo ambayo kwayo unapatikana umoja katika uhalisia wa nje. Hakika kupanga misimamo na kuzalisha maarifa yenye kuisaidia, na kuhamasisha watu wa umma kuelekea huko, ndio mambo ambayo yanahamisha mazungumzo ya umoja kutoka katika kiwango cha hisia na mitazamo na kwenda kwenye kitendo na uhalisia. Na pengine kati ya mambo muhimu sana ambayo ni wajibu kupanga ni misimamo ifuatayo:

Kwanza: Msimamo dhidi ya wingi wa madhehebu ya kiitikadi na kifiqihi, ambapo hakuna uhalisia wa pendekezo lolote la umoja linalofuta upande wowote kati ya pande za umma, au linalotoa masharti ya upande fulani kuachana na itikadi zao na misingi yao, baada ya kujisalimisha katika misingi ya imani na nguzo za Kiislamu, hivyo ni lazima kutangaza wazi kuwakubali wengine katika duara la Uislamu na umma.

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 30 10/26/2015 1:14:49 PM

Pili: Kupinga vitendo vya kukejeli na kuzivunjia heshima alama na matukufu yanayoheshimiwa katika madhehebu yoyote kati ya madhehebu, hakika kukhitalifiana katika kuwakosoa waliotangulia na kuchambua matukio ya zama za mwanzo za Kiislamu kuko ndani ya haki ya kutofautiana katika itikadi na imani, na ni katika yanayokubalika katika wigo wa utafiti wa kielimu, lakini hakutoi kisingizio kwa upande wowote ule kufanya uadui na kejeli dhidi ya alama na matukufu ya upande mwingine.

Tatu: Kukemea tofauti za kiubaguzi katika nchi yoyote na jamii yoyote ya Kiislamu. Haisihi kunyamazia siasa za ubaguzi ambazo zinazuia wafuasi wa madhehebu yoyote ya Kiislamu kufanya ibada zao za kidini na za kimadhehebu au kuwanyima kuneemeka kwa haki zao za uraia.

Nne: Kushajiisha hali ya mawasiliano na mikusanyiko ya kijamii baina ya watu wa umma pamoja bila kujali madhehebu yao, na kuivuka hali ya utengano na ubaguzi katika shughuli za kielimu, kiutamaduni, kisiasa na kijamii, yaani kuacha kuwahamasisha juu ya chuki na bughudha.

Naona kwamba ipatikane mifano ya misimamo hii katika mazungumzo ya umoja. Tulinganie katika kupatikana kwake na tujisukume kwenye kujitolea kivitendo ambako kutaimarisha umoja. Na mwisho wa ulingano wetu ni kwamba shukurani zote ni za Mwenyezi Mungu Mola mlezi wa viumbe.

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 31 10/26/2015 1:14:49 PM

UFUATILIAJI WA MATANGAZO

“Kufanya Ijtihadi katika mazungumzo ya Kiislam ili kuelekea kwenye mazungumzo mapya ya kibinadamu.”

MAULAMAA: Mazungumzo ya Kiislamu yanakabiliwa na tatizo na ni lazima kulizoea na kuliweka wazi.[13]

Doha – Muhammad Izaam:

Maulamaa wanasharia na wanafikra wa Kiislamu wameafikana kwamba mazungumzo ya Kiislamu yanakabiliwa na tatizo na inahitaji “kulizoea” na kulikabili katika ulimwengu mzima.

Maulamaa walioshiriki wametia mkazo katika hitimisho la kongamano la “Kufanya Ijtihadi katika mazungumzo ya Kiislam ili kuelekea kwenye mazungumzo mapya ya kibinadamu” ambalo liliandaliwa na kitivo cha sharia na masomo ya Kiislamu katika chuo kikuu cha Qatar, kwa kushirikiana na kitivo cha sharia cha masomo ya Kiislamu katika taasisi ya Qatar – kwamba matatizo makubwa ya mazungumzo yanajikita katika kutofautiana mtazamo wa wasimamizi wake, na kutengeneza mifumo yake, na kiwango cha uchambuzi wake, na uhuru wake kutokana na utawala, na taasisi za kisiri, kwa kuongezea kwenye ubaguzi wa baadhi ya wasimamizi wake na kushadidia kwao madhehebu.

Na wanafikra wamelingania kumaliza hali ya mgawanyiko ambayo inakabili mazungumzo na siasa za ubaguzi, vita vya ikhitilafu na fitina, na kuunganisha baina ya fiqihi na malezi kwa wasimamizi wa mazungumzo na kutoghafilika nayo kupitia ufahamu wa makusudio. Na Dr. Mudhir Qahfu amelingania tangu mwanzo wa kikao cha

[13] Jarida la al-Arab la Qatar toleo la 7989 la Jumanne 13/ 5/1431 Hijiria sawa na 27/4/2010.

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 32 10/26/2015 1:14:49 PM

jana kwenye utandawazi wa mfumo wa msaada wa kiuwezeshaji wa Kiislamu na kuutoa kwa ulimwengu kana kwamba ni njia ya msaada wa kibinadamu kwa ujumla, unaoundwa kutokana na kanuni zinazopangilia malengo maalum yanayofungamanishwa na nyanja za kiuchumi na maisha ya jumla hadi ubadilike na kuwa ni mfumo wa kiulimwengu unaofaa kwa watu wote, nao ndio unaoendana pamoja na mtazamo wa Kiislamu ambao unasimama kama ni rehema kwa walimwengu.

Na Qahfu amezielezea benki za Kiislamu kuwa ni za ulimbikizaji, kwa kuona kwamba zinalazimisha kwa wateja wake mfumo wa benki zinazobebesha miamala kwa namna ambayo inazidi benki za kawaida, kama ambavyo zinalazimisha bei zake kwa watumishi wake kwa kusema: "Matumizi ya Kiislamu si uchumi wa Kiislam." Na kuhusu mfumo wa wakfu, Qahfu amesema: "Hakika wakfu ulitengenezwa na Waislamu ili kuepukana na kibano cha serikali, lakini kwa mara nyingine tumeutoa zawadi kwa serikali." Na ametaka kufahamu uendeshaji wa wakfu ili kulinda maslahi ya umma na kusaidia uhuru wa maamuzi yake na mazungumzo yake kutokana na watawala.

Na Dr. Hasan as-Saffar (mtafiti) amesema: "Hakika mazungumzo ya umoja ya kileo yanakabiliwa na changamoto nyingi za hatari ambazo zinaonekana katika hali ya mgawanyiko, siasa za ubaguzi, vita vya ikhitilafu, fitina na kusambaa sana maneno ya uchochezi na chuki za kimakundi, ambapo sio tu khutuba katika msikiti au Husainiya na wala sio tu kitabu kilichochapishwa, bali imekuwa ni tangazo linalovuka mabara kupitia runinga, vituo vya tovuti na huduma za simu za mikononi, huku kukiwepo na udhaifu katika khutuba za umoja kwa madai ya kuboresha na kuendeleza, udhaifu unaozuia mwitikio, na mazungumzo mengi yanakabiliwa na hali ya kudumaa na kutuama katika madhumuni yake, na katika

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 33 10/26/2015 1:14:49 PM

mbinu ambazo wanazitumia, na katika kiwango cha harakati na uwezo wa kuathiri."

Na as-Saffar ametilia mkazo kwamba mazungumzo ya umoja yanakabiliwa na upungufu mkubwa katika upande wa idadi na aina, na amesema mukabala wa mamia ya taasisi na mimbari za matangazo na utamaduni unaozalisha chuki za kibaguzi, na wasambazaji wa mitazamo ya kasumba za kimadhehebu, hakuna isipokuwa idadi ndogo ya taasisi zinazojali mazungumzo na mambo ya umoja kati ya makumi ya maelfu ya maulamaa wa kidini na wanaojinasibisha na dini miongoni mwa makhatibu na walinganiaji. Na kati ya makumi ya maelfu miongoni mwa maulamaa wa kidini na wanaojihusisha na masuala ya dini kati ya makhatibu na walinganiaji, ni wachache tu miongoni mwao ndio wenye kubeba jukumu la kueneza umoja na kupambana na utamaduni wa ikhitilafu na mpasuko. Na lau tukichunguza harakati za vitabu na usambazaji wa makala tutakuta kwamba kiashirio cha uzalishaji na usambazaji wa maandishi ya ubaguzi wa kimadhehebu uko juu zaidi ukilinganisha na idadi ndogo ya maandishi yanayolingania umoja na mshikamamo. Saffar amezitaka taasisi za kiraia kujali suala la kusambaza utamaduni wa umoja na usamehevu, na kuongoza kujitolea kuzima moto na kuhamasisha majadiliano baina ya pande mbalimbali ili kudumisha utulivu na amani ya jamii."

As-Saffar amehadharisha kwamba mazungumzo ya ubaguzi yanazungumza kwa sauti ya juu na kujiamini kukubwa wakati ambapo mazungumzo ya umoja mengi miongoni mwayo yanasifika kwa kiasi kikubwa kwa kuona aibu na haya na amesema: "Katika upande wa ulinganisho baina ya kiwango cha utekelezaji baina ya khutuba mbili, hakika mazungumzo ya ubaguzi yanamiliki uwezo wa kuathiri kwa watu na kuamsha hisia zao na hamasa zao, na kuwasukuma kuiendea fitina na vita na ugomvi mkubwa zaidi, wakati

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 34 10/26/2015 1:14:49 PM

ambapo harakati za mazungumzo ya umoja zinakaribia kuwa ni za jopo dogo, jambo ambalo linahitajia utafiti katika hoja za mazungumzo ya umoja na mbinu za kuzungumza na watu wa umma, na upeo wa uwezo wa kuathiri kwake katika kuamsha hisia nzuri na hisia za kujenga ndani ya nafsi za watu wa umma, kwa ajili ya maslahi ya kuelekea kwenye umoja na misimamo ya amani na ulewano."

Na Saffar ameashiria kwamba lengo la msingi la mazungumzo ya umoja ni kusahihisha uhusiano baina ya makundi na pande za jamii ya Kiislamu, na kuihami kutokana na mizozo na mpasuko, ili iishi kwa utulivu na amani ya ndani, na kuelekea kwenye ustawi na maendeleo kwa kutumikia maslahi makuu na kukabiliana na changamoto hatari. Na Saffar amelingania katika kujenga dhana ya Uraia na dhana ya Haki za Binadamu ili kumaliza anwani ya mzozo na mpasuko na mianya ya fitina katika hali ya umma wa kileo, na ili kutatua mas'ala ya ubaguzi kupitia kukubali usawa baina ya wananchi na kuondoa ubaguzi wa kimakundi, na haya ndio madhumuni ya uraia kwa dola kuangalia wananchi wake kama wananchi kabla ya kitu kingine chochote, na kwa kufumbia macho anwani zao nyingine za pembezoni.

Saffar amesisitiza kwamba mazungumzo ya umoja yanahitaji kupanga msimamo kuhusiana na wingi wa madhehebu ya kiitikadi na kifiqihi, ambapo hakuna ukweli wa pendekezo lolote la umoja la kufuta upande wowote kati ya pande za umma, wala hakuna yeyote anayetoa sharti la wengine kuacha itikadi zao na imani yao baada ya kukubali misingi ya imani na nguzo za Kiislamu. Ni lazima kutangaza wazi kuwakubali wengine ndani ya duara la Uislamu na umma, kwa kuongezea kupinga vitendo vya kuzifanyia kejeli alama na matukufu yanayoheshimiwa na madhehebu yoyote miongoni mwa madhehebu kwa kusema: "Hakika kukhitalifiana katika kuwakosoa waliotangulia na kuchambua matukio ya zama za mwanzo za Kiis-

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 35 10/26/2015 1:14:49 PM

lamu kuko ndani ya haki ya kutofautiana katika itikadi na imani, na ni katika yanayokubalika katika wigo wa utafiti wa kielimu, lakini hakutoi kisingizio kwa upande wowote ule kufanya uadui na kejeli dhidi ya alama na matukufu ya upande mwingine."

Saffar ametaka kukemea ubaguzi wa kimakundi katika nchi na jamii yoyote ya Kiislamu, na akasema: "Haisihi kunyamazia siasa ya ubaguzi ambayo inazuia wafuasi wa madhehebu yoyote ya Kiislamu kufanya ibada zake za kidini na kimadhehebu au kuwanyima kufurahia haki zao za kiraia." Saffar amesisitiza dharura ya kushajiisha hali ya mawasiliano ya kijamii baina ya watu wa umma pamoja na kutofautiana madhehebu yao na kuvuka hali ya utengano na kubaguana katika shughuli za kielimu, kiutamaduni, kimatangazo, kisiasa na kijamii na kukemea uhamasishaji wowote wa chuki na bughudha.

Ama Dr. Saifu Abdul-Fataha – Profesa wa elimu ya siasa katika chuo kikuu cha Cairo – amekazia katika dhana ya utawala bora, na uhusiano wake na dhana ya mazungumzo ya Kiislamu. Abdul-Fataha ameashiria kwenye utawala bora kwa mifano ya utawala na misingi ya Shura inayofuatwa na vipimo vya ukweli na uwazi, kwa yale yanayoendeleza uhusiano baina ya dola na watu wa jamii, na dhana yake itimie katika kutengeneza maana ya sharia na rejea halisi katika mazungumzo ya Kiislamu.

Na amesema Daktari Hatim al-Qaranshawiy, mkuu wa kitivo cha sharia na masomo ya Kiislamu, katika hitimisho la kikao: "Hakika mazungumzo ya Kiislamu yanakabiliwa na tatizo kwa sababu ya kutofautiana mtazamo wa wawasilishaji wake, kama ambavyo sisi tunahitaji majadiliano ndani ya kila madhehebu ili kuyaunganisha na majadiliano baina ya madhehebu." Na ameashiria kwamba baadhi ya wanafikra wameashiria kwamba mazungumzo yamejitenga yenyewe katika ufafanuzi na kujiepusha mbali na mambo ya umma na jamii kwa kusema: "Ndani ya mazungumzo kuna wanaoamini

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 36 10/26/2015 1:14:49 PM

harakati pamoja na maisha ya jamii, na kuna wanaopinga na wanapendelea kujitenga.”

Na Daktari Hasan Hanafiy, Ustadhi wa falsafa katika chuo kikuu cha Cairo, katika kuhitimisha maneno yake: “Hakika lugha ya mazungumzo ya Kiislamu haiwezi tena kukabiliana na changamoto za kisasa.” Na amelingania kutengeneza mazungumzo ya Kiislamu yenye kusheheni hoja na dalili na ziwe huru kutokana na utawala na asasi za kisiri.

Ama Daktari Sultwani al-Hashimiy amesema: “Hakika tatizo la mazungumzo limejikita baina ya maulamaa na walinganiaji watendaji na wale maulamaa wangojeaji, kwa sababu wale wangojeaji hawawezi kuainisha uhalisia, ambapo ni tofauti na wale maulamaa watendaji.” Na amelingania ushirikiano baina ya wawili hao kwa ajili ya maslahi ya umma.

Inaelezwa kwamba mkutano uliandaliwa kwa ushirikiano baina ya kitivo cha masomo ya Kiislamu, ambacho ni mwanachama wa taasisi ya mafunzo ya Qatar, na kitivo cha sharia na masomo katika chuo kikuu cha Qatar kwa ajili ya kuleta ukuruba baina ya elimu za kibinadamu na kijamii katika upande mmoja na elimu ya sharia ambayo inazingatia ijitihadi ya kifiqihi.

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 37 10/26/2015 1:14:49 PM

AMESISITIZA KWAMBA HAKUNA UKWELI WOWOTE WA PENDEKEZO LA UMOJA UNAOTOA SHARTI LA WENGINE KUACHA ITIKADI ZAO

Mwanachuoni wa Kishia wa Kisaudi ameshtumu siasa za ubaguzi na za kimakundi na ametaka kukabiliana nazo.[14]

London: Al-Qudusi al-Arabiy:

Mwanachouni wa kidini wa Kishia wa Kisaudia Sheikh Hasan Saffar ameshutumu siasa za ubaguzi na za kimakundi katika nchi za Kiarabu, ametoa wito wa kutatua mas'ala ya kibaguzi kupitia kukubali usawa na kuondoa matatizo yote ya ubaguzi baina ya wananchi. Saffar amesema katika kushiriki kwake katika kongamano la "Kufanya Ijtihadi katika mazungumzo ya Kiislam ili kuelekea kwenye mazungumzo mapya ya kibinadamu" ambalo lilimalizika katika mji mkuu wa Qatar mwishoni: "Haisihi kunyamazia siasa za ubaguzi ambazo zinazuia wafuasi wa madhehebu za Kiislamu kufanya ibada zao za kidini na kimadhehebu au kuwanyima kufurahia haki zao zote za kiraia."

Na katika mahudhurio makubwa ya Maulamaa kutoka madhehebu mbalimbali za Kiislam Saffar amehadharisha hatari ya Maulamaa wa kidini kuendelea katika uchochezi wa ubaguzi kupitia mimbari za kidini. Hii ni kwa mujibu wa tovuti ya habari ya Raswid ya Kishia ya Saudia. Na amefafanua kwamba lengo la msingi la mazungumzo ya umoja ni kusahihisha uhusiano baina ya makundi ya jamii ya Kiislam, na kuihami kutokana na mizozo na mpasuko ili kuishi kwa

[14] Jajarida la Qudusi la Kiarabu toleo la 6498 linalotolewa London la siku ya ijumaa, 16 Jumadil-Ulaa 1341 Hijiria, sawa na 30 April 2010.

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 38 10/26/2015 1:14:50 PM

utulivu na amani ya ndani, na kuelekea kwenye ustawi na maendeleo kwa kutumikia maslahi makuu, na kukabiliana na changamoto hatari. Na ameongezea: "Hakuna uhalisia wa pendekezo lolote linalotoa sharti la wengine kuacha itikadi zao na imani zao, ni lazima kutangaza wazi kuwakubali wengine ndani ya duara la Kiislam la umma." Na amesisitiza katika mazungumzo yake kupinga kitendo cha kukejeli na kuzivunjia heshima alama za madhehebu mengine. Na akasema: "Hakika kukhitalifiana katika kuwakosoa waliotangulia na kuchambua matukio ya zama za mwanzo za Kiislamu kuko ndani ya haki ya kutofautiana katika itikadi na imani, na ni katika yanayokubalika katika wigo wa utafiti wa kielimu, lakini hakutoi kisingizio kwa upande wowote ule kufanya uadui na kejeli dhidi ya alama na matukufu ya upande mwingine."

Na kulingana na waraka alioutoa katika mkutano ambao ulifunguliwa kwa khutuba ya Sheikh Yusufu al-Qaradhwawiy, as-Saffar alisema: "Hakika kuna uchache wa Maulamaa wa kidini wanaojali mazungumzo ya umoja wakati ambapo wengi bado wangali wako katika upande wa uchochezi wa kibaguzi na kasumba za kimadhehbu." Ameongezea kwa kusema kwamba kati ya maelfu ya maulamaa wa dini na makhatibu na walinganiaji "Hatukuti miongoni mwao isipokuwa wachache tu kati ya watu wanaojali kusambaza mazungumzo ya umoja." Na amekosoa mazungumzo ya kidini yanayosifika kwa sifa ya kuiga, kudumaa na kunyamaza, ukilinganisha na mazungumzo ya uchochezi na uhamasishaji wa ubaguzi ambayo yamekuwa ni tangazo linalovuka mabara kulingana na maneno yake.

Saffar amesema: "Hakika mazungumzo ya ubaguzi yanazungumzwa kwa sauti ya juu wakati ambapo mazungmzo mengi ya umoja kiasi kikubwa yanazungumzwa kwa kuona aibu na haya." Na ameeleza kuhusu itikadi yake kwamba mazungumzo ya ubaguzi yanamiliki uwezo mkubwa zaidi wa kuathiri kwa watu na kuamsha

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 39 10/26/2015 1:14:50 PM

hisia na kuwaingiza wao katika fitina na mapambano ya kivita. Na ametaka mukabala wa hayo kuunda taasisi za kiraia zitakazoshughulika na kusambaza utamaduni wa umoja na usamehevu na kuongoza katika kuzika fitina na kuzima moto na kushajiisha majadiliano baina ya wanaotofautiana ili kuimarisha amani ya jamii.

Na umekuja mkutano ambao uliandaliwa na kitivo cha masomo ya Kiislamu katika Chuo Kikuu cha Qatar kwa muda wa siku tatu katika mtiririko wa kupunguza pengo baina ya elimu za kibinadamu na kijamii katika upande mmoja, na elimu za kisharia ambazo zinajali ijitihadi ya kifiqihi katika upande mwingine.

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 40 10/26/2015 1:14:50 PM

REJEA

1. حيدر حب الله. مسألة المنهج في الفكر الديني.

2. حمد بن جرير الطبري. تاريخ الطبري، الطبعة الخامسة 1409،(بيروت: مؤسسة الأعلمي للمطبوعات.)

3. الخطيب البغدادي. تاريخ بغداد،(بيروت:دار الكتب العلمية).

4. علاء الدين علي المتقي بن حسام الهندي. كنز العمال. الطبعة الخامسة 1405،(بيروت: مؤسسة الرسالة).

5. ابن عبد البر. جامع بيان العلم، طبعة المنيرية.

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 41 10/26/2015 1:14:50 PM

6. يوسف القرضاوي. الصحوة الإسلامية بين الاختلاف المشروع والتفرق المذموم، الطبعة الثالثة 1414 (بيروت: همؤسسة الرسالة).

7. حجة الله البالغة، للدهلوي. طبعة مصر 1352.

8. ابن كثير الدمشقي. البداية والنهاية، الطبعة الأولى 1421، ه (بيروت: دار الكتب العلمية).

9. محمد ناصر الدين الألباني. صفة صلاة النبي من التكبير إلى التسليم كأنك تراها، الطبعة السادسة 1391، (بيروت: ه المكتب الإسلامي).

10. محمد عيد عباسي. بدعة التعصب.الطبعة الثانية 1406، 1 ه (عمان: المكتبة الإسلامية).

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 42 10/26/2015 1:14:50 PM

ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 43 10/26/2015 1:14:50 PM

57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a)
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenye kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
100. Idi Al-Ghadir
101. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
102 Hukumu zinazomhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Kumsalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqalain
115. Ndoa ya Mutaa
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 44 10/26/2015 1:14:50 PM

119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Mkutano wa Maulamaa wa Baghdad
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Elimu ya Ghaibu ya Maimamu
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu
135. Yafaayo kijamii
136. Tabaruku
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
153 Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur’an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur’an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Qur’ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Je, Kufunga Mikono
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas’ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur’ani
178. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya ‘Alaa Khayri’l-’Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 45 10/26/2015 1:14:50 PM

181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Maswali Ya Uchunguzi Kuhusu Uislam
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye
189. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Upotoshaji dhahiri katika Turathi (Hazina) ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina (‘as) na Makhalifa
197. Uongozi na Utawala katika Mwenendo wa Imam ‘Ali (‘a)
198. Kuvunja hoja iliyotumika kutetea Uimamu wa AbuBakr
199. Adabu za vikao na mazungumzo
200. Hija ya Kuaga
201. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo
202. Fadhila za watukufu watano katika Sahih Sita
203. Mdahalo baina ya Mwanachuoni wa Kisunni na Mwanachuoni wa Kishia (*Al-Muraja’aat*)
204. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (as)
205. Mjadala wa Kiitikadi
206. Mtazamo kuhusu msuguano wa Kimadhehebu
207. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
208. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah juu ya Imam Ali (as)
209. Uongozi wa Kidini – Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii
210. Maadili ya Ashura
211. Mshumaa – Shahidi na Kifo cha Kishahidi
212. Mizani ya Hekima – Hadithi za Ahlul Bait (as) – Sehemu ya Kwanza
213. Imam Ali na Mambo ya Umma
214. Imam Ali na Mfumo wa Usawa
215. Mwanamke na Sharia
216. Mfumo wa Wilaya
217. Vipi Tutaishinda Hofu?
218. Kumswalia Mtume ni Ufunguo wa Utatuzi wa Matatizo
219. Mahali na Mali za Umma
220. Nahjul-Balagha – Majmua ya Khutba, Amri, Barua, Risala, Mawaidha na Semi za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib (a.s.)
221. Mukhtar – Shujaa aliyelipiza kisasi dhidi ya wauaji wa Imam Husein (as) hapo Karbala
222. Uimamu na Tamko la Kutawazwa
223. Imam Husain ni Mfumo wa Marekebisho na Mageuzi
224. Saada Kamili – Kitabu cha Kiada cha Maadili
225. Maeneo ya Umma na Mali Zake
226. Imam Hasan na Mfumo wa Kujenga Jamii
227. Adhana ni Ndoto au ni Wahyi?
228. Maimamu wa Ahlul Bait – Ujumbe na Jihadi

KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba’Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n’amavuko by’ubushiya
4. Shiya na Hadithi.

ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION KWA LUGHA YA KIFARANSA

1. Livre Islamique

04_15_Mazungumzo ya umoja_26_Oct_2015.indd 46 10/26/2015 1:14:50 PM